
Kata ya Kashashi, Wari, Orkolili.
Alisema shirika hilo linadai sh.

badala yake hutegemea fedha za bili

**MGAWO**

UHURU UK 6.



**WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (mwenye miwani), akiwagawia wananchi samaki aliowanunua katika Soko la Deep Sea, jijini Tanga, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo, jana.** (Na Mpigapicha Wetu).

# Mpina awashtukia wanaoshusha thamani ya maziwa

**Na LILIAN JOEL,** *Arusha*

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amekiagiza Kiwanda cha Galaxy Food and Beverage Ltd, kilichoko Jijini Arusha, kudhibiti viwango vya bei ili kuondoa hujuma za kiabiashara zinazofanywa na wajanja wachache wanaoshusha thamani ya maziwa yanayozalishwa nchini.

Akizungumza juzi, Jijini Arusha, alipotembelea kiwanda hicho kwa ajili ya kujionea uzalishaji wa maziwa, Mpina alisema serikali imeweka mazingira rafiki ya biashara ili maziwa yanayozalishwa nchini yawe na soko zuri popote yanapouzwa.

"Katika bajeti ya serikali ya mwaka 2020/2021, kupitia Wizara ya Fedha, tumeondoa tozo na kodi mbalimbali ili kuwezesha uwekezaji wa aina hii uwe na tija na matokeo chanya nchini.

"Hivyo tozo na kodi siyo tatizo, tena na huu ni wakati wenu mwafaka kuhakikisha mnapanua wigo wa biashara yenu kwa nchi nzima, hizi asilimia 70, hazitoshi zifike 100," alisema.

Kwa mujibu wa Mpina, maziwa yanayozalishwa na kiwanda hicho yana ubora mzuri, hivyo ni vyema yakasambazwa mikoani, hasa kwenye majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya na mikoa mingine.

"Mifumo ya bei inapaswa kuangaliwa kwa ukaribu ili wauzaji maziwa kwa mawakala, wauze kwa bei nafuu na hata yale ya sokoni, bei iwe nzuri ili tutofautishe na maziwa yanayotoka nje ya nchi," alisema Mpina.

Waziri huyo alikipongeza kiwanda hicho kwa kununua maziwa kwa wafugaji kwa bei inayoridhisha ya zaidi ya sh. 800 na kuzingatia kipaumbele cha serikali cha kutaka bei za bidhaa hizo ziwe nafuu.

Kwa upande wake, Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa, Noely Byamungu, alisema uwepo wa kiwanda hicho ni muhimu katika kukuza uchumi wa wafugaji nchini.

"Kazi ya bodi hiyo ni kusimamia, kuratibu na kuongeza thamani maziwa pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji ili wafuge kisasa na kupata maziwa ya kutosha,"alisema.

Naye, Ofisa Mwendeshaji katika kiwanda hicho, Hasheem Said, alisema maziwa yanayoletwa kiwandani hapo, yanapimwa kikamilifu kwa ajili ya kuhakiki ubora wake, kabla ya kuanza kusindikiwa kiwandani.

Said, aliiomba serikali kuendelea kusimamia sera ya unywaji wa maziwa, ili kuongeza idadi ya Watanzania wanaotumia bidhaa hiyo na kuongeza uzalishaji viwandani.

**Bei**

**MIFUMO IANGALIWE**

Mifumo ya bei inapaswa kuangaliwa kwa ukaribu ili wauzaji maziwa kwa mawakala, wauze kwa bei nafuu na hata yale ya sokoni, bei iwe nzuri ili tutofautishe na maziwa yanayotoka nje ya nchi,"

Scanned with CamScanner

kuondokana na tatizo la njaa," alisema na kuwaomba wakulima kuchangamkia fursa hiyo.

NIPASHE UK9.

# Wavuvi kukopeshwa kudhibiti uvuvi haramu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya Kilimo (TADB), Japhet Justine, amemhakikishia Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi hususani wa Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuondokana na uvuvi haramu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ziara alipotembelea Bwawa la Nyumba ya Mungu na kujionea shughuli zinazofanywa na wavuvi akiwa na Waziri Mpina, Justine alisema benki hiyo imedhamiria kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya uvuvi kwa kuwawezesha wavuvi zana za kisasa.

"Kumekuwa na matumizi ya zana zisizo na ubora katika shughuli za uvuvi, hali ambayo imesababisha mazalia ya samaki kupungua na kuzorotesha mapato katika sekta hiyo, TADB tutaendelea kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu wavuvi ili kuwa na uvuvi endelevu kote nchini," alisema.

Justine alisema milango ipo wazi kwa benki na taasisi za fedha kushirikiana na benki hiyo ili kupunguza changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi na ufugaji ambazo zimeajiri Watanzania wengi.

Waziri Mpina alipongeza hatua zinazochukuliwa na TADB na kuwataka wavuvi kutumia vyema mikopo inayotolewa na benki hiyo ili kuleta maendeleo ya kweli hapa nchini.

"Rasilimali za uvuvi zinatakiwa kulindwa na kila mwananchi, tunaipongeza TADB kwa uzalendo wao wa kuwawezesha wavuvi ili kuondokana na uvuvi wa kutumia zana hafifu ambazo zimeleta athari hasi katika sekta hii kwa kupunguza mazalia ya samaki," alisema Mpina.

ziara ya kukagua miradi ya maendeleo jijini Arusha,

Alisema serikali imejenga shule nyingi pamoja na

Kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Arusha

wa maeneo ya jirani na hospitali hiyo wame-

Shule ya Seku ukiendelea.

HABARI LEO UK 15.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo akimuonesha Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk Rashid Tamatamah (aliyekaa) namna kiwanda hicho cha kuchakata samaki kitavyokuwa kinaonekana baada ya kukamilika kwa ukarabati wake, wakati wa ziara yake kiwandani hapo mkoani Rukwa juzi. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi wa wizara hiyo, Stephen Lukanga. (Na Mpigapicha Wetu).

# Wak wala mbeg na u

Na Lucy

W otumia k hali amb kilimo c Msin Kituo c Teknolo Kilimo kutoka wa Ki Isabel alipol Haba H char liwa kituo kusa na ku utafi bali w na ka mbeg kilim A kumu mkul



...(Na Mpigapicha Wetu).

HABARI LEO UK 17.

# Mpina aagiza kiwanda kudhibiti viwango vya bei

**Na Veronica Mheta, Arusha**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina amekiagiza Kiwanda cha Galaxy Food and Beverage Limited, kuhakikisha kinadhibiti viwango vya bei, ili kuondoa hujuma za kibiashara zinazofanywa na wajanja wachache na kushusha thamani ya maziwa yanayozalishwa nchini.

Akizungumza jijini Arusha juzi wakati alipotembelea kiwanda hicho kwa ajili ya kujionea uzalishaji wa maziwa, Mpina alisema serikali imeweka mazingira rafiki ya biashara ili kuwezesha maziwa yanayozalishwa nchini kuwa na soko zuri popote yanapouzwa.

"Katika bajeti ya serikali ya mwaka huu, kupitia Wizara ya Fedha, tumeondoa tozo na kodi mbalimbali ili kuwezesha uwekezaji huu kuendelea kuleta tija na matokeo chanya hapa nchini, hivyo tozo na kodi sio tatizo tena sasa jipanueni nchi nzima hizi asilimia 70 hazitoshi fikisheni 100," alisema.

Alisema maziwa yanayozalishwa na kiwanda hicho ambayo hufahamika kwa jina la Tanga Fresh, yana ubora ambao unatakiwa huku akiwataka kupeleka bidhaa hiyo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na masoko yote ya ndani, kwa kuwa uhitaji ni mkubwa.

"Mifumo ya bei inapaswa kuangaliwa kwa ukaribu ili wauzaji maziwa kwa mawakala wauze kwa bei nafuu na hata yale ya sokoni bei iwe nzuri ili tutofautishe na maziwa yanayotoka nje ya nchi," alisema.

Mpina alikipongeza kiwanda hicho kwa kununua maziwa kwa wafugaji kwa bei inayoridhisha ya zaidi ya Sh 800 na kuzingatia kipaumbele cha serikali cha kutaka bei za bidhaa hizo ziwe nafuu.

Kwa upande wake, Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa, Noely Byamungu alisema uwepo wa kiwanda hicho ni muhimu katika kukuza uchumi wa wafugaji na nchi.

Pia alisema kazi ya bodi hiyo ni kusimamia, kuratibu na kuendeleza tasnia ya maziwa na wafugaji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wafugaji wanafuga kisasa na kuzalisha malighafi zenye ubora unaohitajika sokoni.

Hasheem Said ambaye yupo katika kitengo cha uendeshaji kiwandani hapo aliipongeza serikali kwa kuanzisha viwanda na kuvifufua vilivyokufa kwani hatua hiyo imesaidia vijana kupata ajira.

Hata hivyo, aliiomba serikali kusimamia sera ya unywaji wa maziwa, ili kuongeza idadi ya Watanzania kutumia bidhaa hiyo na kuongeza uzalishaji viwandani.

Scanned with CamScanner

MAJIRA UK 2.

# Toeni taarifa migogoro ya wakulima, wafugaji mapema

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina ametaka wananchi wa Kijiji cha Kidoka wilayani Chemba mkoani Dodoma watoe taarifa kwa wakati zinazohusu migogoro ya wakulima na wafugaji ili Wizara yake iweze kuifanyia kazi.

Waziri Mpina aliyasema hayo alipotembelea kijiji hicho akiwa na lengo la kusikiliza changamoto za wafugaji ili ziweze kufanyiwa kazi ambapo changamoto nyingi zilizotajwa na wafugaji hao zinahusisha wizara mbalimbali ikiwa ni Pamoja naWizara ya Nishati,Ardhi na Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Akianisha Changamoto hizo mwananchi mfugaji wa kijiji hicho Abuu Mikidadi amesema kijiji hicho kinakabiliana na changamoto ya eneo la malisho ya mifugo,ambapo kulikuwa na eneo la wazi lilitengwa kwa ajili ya malisho lakini limevamiwa na wakulima ambapo wafugaji wakiingiza mifugo yao wanavamiwa na kupigwa.

Alisema pia kuna changamoto ya josho la kuogeshea mifugo ya pamoja na pembejeo za mifugo,Akijibu hoja hizo Waziri Mpina alisema Serikali ni moja na inafanya kazi kwa kushirikiana,hivyo hawezi kuyakimbia matatizo hayo na atahakikisha anafikisha ujumbe kwa Wizara nyingine. "Tunayo kazi ya kufanya kama Serikali kuangalia namna gani changamoto hizi zinaweza kut atuliwa kama vile kupunguza gharama za umeme kwa kuzungumza na Tanesco kuweza kushusha tariffs ili wakulima na wafugaji kijijini hapo waweze kufanyakazi bila gharama yoyote na serikali imepunguza tozo za kuogeshea mifugo naitaleta pembejeo za mifugo na kuuzwa kwa bei elekezi," alisisitiza.

Waziri Mpina aliendelea kusema: "Kuna haja ya kukaa na Waziri wa Kilimo, kuangalia huu mradi wa Umwagiliaji Chemba unaolalamikiwa na wakulima na wafugaji unawezaje kuboreshwa ili wananchi wapate faida."

Mpina alishauri viongozi wa serikali ya kijiji na serikali ya wilaya wakae ili waweze kupata suluhisho.

Sambamba na hilo alisema: "Nitaleta timu inayoshugulikia migogoro toka wizarani kwangu pamoja na wataalam waje hapa kutafuta majawabu yasiyo na upendeleo, asidhulumiwe mtu yoyote asinyanyaswe mtuyeyote, kila mtua pate haki yake na wataleta mapendekezo serikalini."

Aliendelea kusema kuwa na hakuna mfugaji anayeruhusiwa kuingiza mifugo kwenye mashamba ya watu wengine, na kuwataka wananchi watoe taarifa kwa wakati kwa wataalam wa kilimo na mifugo na kwa jeshi la Polisi. "Hatuwezi kuwa na mfugaji anayedharau shughuli za wengine na hakuna anayeweza kuishinda serikali," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilayaya Chemba Dkt. Semistatus Mashimba alisema kufuatia changamoto ya matumizi makubwa ya umeme wananchi waliomba serikali kwa kupitia shirika la umeme nchini TANESCO kuwaunganisha na umeme wa Solar ambapo mapendekezo hayo yanafanyiwa kazi yakienda sambamba na kuangalia uwezekano wa wananchi hao kuhamishiwa katika tariff ndogo ili waweze kumudu gharama.

Kwa upande wa kuuza mazao ya wakulima, Mkurugenzi huyo alisema serikali hailazimishi mkulima yoyote kuuza mazao kwa mfumo wastakabadhi ghalani bali mkulima yupo huru kupeleka mazao popote anapotaka.

Waandishi

Scanned with CamScanner

MWANANCHI UK 24



# Kiwanda chatakiwa kuzalisha zaidi

**Husna Issa**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**"Soko la bidhaa zenu ni kubwa, hivyo ni lazima muongeze uzalishaji na msambaze dawa maeneo mengi chini."**
**Mpina**

**Arusha.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina ameagiza uongozi wa kiwanda cha kuzalisha dawa za mifugo, viatilifu na vifungashio cha Farm Access LTD , kuongeza uzalishaji kutoka asilimia 20 ya sasa na kufikia silimia 100 ili kukidhi mahitaji ya mifugo nchini.

Akizungumza jana alipotembelea kiwanda hicho kilichopo Ngaramtoni nje kidogo ya jiji la Arusha, alisema iwapo kiwanda hicho kitakidhi malengo kitaisaidia Serikali kupunguza gharama za uagizaji dawa za mifugo nje ya nchi.

"Soko la bidhaa zenu ni kubwa, hivyo ni lazima muongeze uzalishaji na msambaze dawa maeneo mengi chini. Jambo hili litasaidia kupunguza matumizi ya fedha nyingi za Serikali kuagiza bidhaa hizi nje ya nchi," alisema .

Awali, Mkurugenzi wa biashara wa kiwanda hicho, Danny Ngowi alisema kiwanda kilianzishwa mwaka 2013 kwa lengo la kuagiza na kusambaza dawa za mifugo kutoka nje ya nchi, lakini kutokana na changamoto ya baadhi ya dawa kutokuwa na ubora wameamua kuanzisha kiwanda hicho na kutengeneza dawa.

Alisema kiwanda hicho kimekuwa cha kwanza kutengeneza na kusambaza dawa za mifugo na viatilifu kwa ajili ya soko la ndani.

Alisema wakati wanaanzisha walipata changamoto ya mtaji kutoka taasisi za fedha, lakini baadaye benki mbalimbali zilionyesha nia ya kutoa fedha za mkopo ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ambayo imesaidia kuinua kiwanda hicho.

Scanned with CamScanner